ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
SPIKA – MHE. PANDU AMEIR KIFICHO

1.Mhe. Kamal Basha Pandu	Naibu Spika/Jimbo la Rahaleo.
2.Mhe. Ali Mzee Ali	Mwenyekiti wa Baraza/Uteuzi wa Rais.
3.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	MBM/Waziri Kiongozi/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mwanakwerekwe.
4.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Naibu Waziri Kiongozi/Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo/ Jimbo la Donge.
5.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	Kiongozi wa Upinzani/"Waziri Kivuli"–Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Mgogoni.
6.Mhe. Haji Omar Kheri	Mnadhimu wa Upande wa Serikali/Jimbo la Tumbatu.
7.Mhe. Haji Faki Shaali	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Katiba na Utawala Bora/Mnadhimu wa Upande wa Upinzani/Jimbo la Mkanyageni.
8.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi/ Jimbo la Dimani.
9.Mhe. Hamza Hassan Juma	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/ Jimbo La Kwamtipura.
10.Mhe. Ramadhan Abdulla Shaaban	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora/Uteuzi wa Rais.

11.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi Vya S.M.Z./Jimbo la Jang'ombe.
12.Mhe. Br.Gen. Adam C. Mwakanjuki	MBM/Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Uteuzi wa Rais.
13. Mhe. Machano Othman Said	Waziri wa Nchi, (AR) Mawasiliano na Uchukuzi./Jimbo la Chumbuni.
14.Mhe. Samia Suluhu Hassan	MBM/Waziri wa Utalii/Biashara na Uwekezaji/Nafasi za Wanawake.
15.Mhe. Burhan Saadat Haji	MBM/Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/ Jimbo la Kikwajuni.
16.Mhe. Asha Abdalla Juma	MBM/Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana,Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais.
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Makunduchi.
18.Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry	MBM/Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/ Uteuzi wa Rais.
19.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Kiembesamaki.
20.Mhe. Zainab Omar Moh'd	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum/ Nafasi za Wanawake.
21.Mhe. Idi Pandu Hassan	Mwanasheria Mkuu wa Serikali.
22. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo/Jimbo la Mpendae.

23. Mhe. Mzee Ali Ussi	Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chaani.
24. Mhe. Khatib Suleiman Bakari	Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Bububu.
25.Mhe. Khamis Jabir Makame	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mtoni.
26.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Dole.
27.Mhe. Tafana Kassim Mzee	Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Uzini.
28.Mhe. Zahra Ali Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/Nafasi za Wanawake.
29.Mhe. Zakiya Omar Juma	"Waziri Kivuli"-Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Nafasi za Wanawake.
30.Mhe. Said Ali Mbarouk	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) na MBLM Fedha na Uchumi/Jimbo la Gando.
31.Mhe. Abdulla Juma Abdulla	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ/Jimbo la Chonga.
32.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) Kazi Maalum/Nafasi za Wanawake.
33.Mhe. Hamad Masoud Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Maji,Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Ole.

34.Mhe. Omar Ali Shehe	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chake-Chake.
35.Mhe. Rashid Seif Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Ziwani.
36.Mhe. Mohamed Ali Salim	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani.
37.Mhe. Asaa Othman Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Wete.
38.Mhe. Aziza Nabahan Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Nafasi za Wanawake.
39.Mhe. Najma Khalfan Juma	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo/Nafasi za Wanawake.
40.Mhe. Muhyddin Moh’d Muhyddin	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji/Jimbo la Mtambile.
41. Mhe. Abass Juma Muhunzi	Jimbo la Chambani.
42.Mhe. Abdulla Mwinyi Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja.
43.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini.
44.Mhe. Ali Denge Makame	Jimbo la Amani.
45.Mhe. Ali Haji Ali	Jimbo la Mkwajuni.
46.Mhe. Ali Moh’d Bakari	Jimbo la Tumbe.
47.Mhe. Ali Suleiman Ali	Jimbo la Kwahani.

48.Mhe. Ame Mati Wadi	Jimbo la Matemwe.
59.Mhe. Ame Ussi Juma	Jimbo la Nungwi.
50.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake.
51.Mhe. Anaclet Thobias Makungila	Jimbo la Fuoni.
52. Mhe. Asha Moh'd Hilal	Jimbo la Magogoni.
53.Mhe. Ashura Abeid Faraji	Nafasi za Wanawake.
54.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Nafasi za Wanawake.
55.Mhe. Dadi Faki Dadi	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba.
56.Mhe. Fatma Abdalla Tamim	Nafasi za Wanawake.
57.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	Jimbo la Mji Mkongwe.
58.Mhe. Haji Mkema Haji	Jimbo la Koani.
59.Mhe. Hasnuu Moh'd Haji	Uteuzi wa Rais.
60.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani.
61.Mhe. Major Juma Kassim Tindwa	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Pemba.
62.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope.
63.Mhe. Mkongwe Nassor Juma	Nafasi za Wanawake.
64.Mhe. Moh'd Kombo Mkanga	Jimbo la Chwaka.
65.Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Unguja.
66.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake.
67.Mhe. Omar Ali Jadi	Jimbo la Kojani.

68.Mhe. Pembe Juma Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Unguja.
69.Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu	Jimbo la Muyuni.
70.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake.
71.Mhe. Said Khelef Ali	Jimbo la Bumbwini.
72.Mhe. Salim Abdulla Hamad	Jimbo la Mtambwe.
73.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni.
74.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni.
75.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde.
76.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Nafasi za Wanawake.

Ndg. Ibrahim Mzee Ibrahim	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi.**

Kikao cha Tano – Tarehe 21 Oktoba, 2009

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kabla sijamwita Katibu ili atuongoze katika shughuli za leo, naomba niwape taarifa kwamba mtakumbuka tulipokuwa katika vikao vyetu vya Kamati ya Uongozi na *Briefing*, tulitoa mashauri kwamba ingefaa Waheshimiwa Wajumbe wote tupate nafasi na fursa ya kwenda kuangalia jengo letu la Baraza la Wawakilishi ambalo penye majaaliwa mwakani mnamo mwezi wa April litafunguliwa.

Tukasema kwamba ingefaa basi wajumbe sote tupate nafasi ya kwenda kukagua pale. Pia tulishauri kwamba ingekuwa vyema zaidi, ukaguzi wetu au ziara yetu pale iambatane na kuwepo kwa mjenzi mwenyewe. Mjenzi ilikuwa aende zake leo, lakini baada ya kupokea taarifa hii akaamua kuahirisha safari ili leo tukubali tukamuone. Kwa sababu ya taratibu na shughuli zetu zilivyo, tukasema kwamba mara baada ya semina ile inayohusu benki ya damu na madawa ya kulevya basi twende pale. Tulipanga kwa makisio mnamo saa 9:00 tukakaguwe na mwenyewe mjenzi atakuwepo, ili kama kuna maneno tumwambie na yeye atatueleza.

Kidiplomasia tulimwambia kwamba Waheshimiwa Wajumbe wana hamu sana ya kuja kukusalimia na kukushukuru. Hayo ndio maelezo ambayo tumempa. Akasema na yeye atapenda kwamba aje asalimiane na nyinyi na pia awashukuruni sana kwa ustahmilivu wenu.

Kwa hivyo, niwaombe sana Waheshimiwa Wajumbe, leo mnamo saa 9:00 tutakwenda pale ili mkaguwe na muone hali inavyoendelea, ili kila mmoja awe na taarifa ya wakati huu masuala yamefikia wapi.

Katibu ataandaa utaratibu kwa wale ambao hawatakuwa na usafiri wa kwendea huko, basi usafiri uwepo wa kutupeleka, ili tukashuhudia kama tulivyoshauriana katika vikao vyetu. Waheshimiwa Wajumbe nakushukuruni sana. *(Makofi)*.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 52

Waheshimiwa Wawakilishi Kupewa Huduma Sawa na Wabunge

Mhe. Ali Abdulla Ali – Aliuliza:-

Hivi sasa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limeanza ujenzi wa Afisi za Waheshimiwa Wabunge majimboni zinazotarajiwa kugharimu Shs. 40,000,000/= millioni. Baadhi ya nyumba hizo tayari zimekamilika kwa mfano; Jimbo la Chake-Chake Pemba na kwa Unguja ni Jimbo la Chaani. Sambamba na hilo zimetengwa fedha kwa ajili ya mfuko wa maendeleo wa Jimbo pamoja na kuwekewa Bima.

(a) Je, Mhe. Waziri suala hili unalifahamu.

(b) Katika Zanzibar kila Jimbo lina Mwakilishi na Mbunge. Kwa kuwa Mbunge amepatiwa huduma hizo huoni kuwa Mwakilishi anadhalilika.

(c) Kwa kuwa serikali zetu zote mbili zina maelewano mazuri. Kwa nini zisikae pamoja zikashauriana ili huduma hizi zitolewe sambamba.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako ninaomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 52 lenye vifungu (a),(b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake, naomba nitowe maelezo mafupi yafuatayo:-

Mhe. Spika, kwanza nampongeza Mhe. Mjumbe kwa kujua kwamba kuna maelewano mazuri katika serikali zetu mbili - Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake namba 52 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, nathibitisha kwamba nafahamu ujenzi wa afisi za Waheshimiwa Wabunge majimboni tayari umeshaanza na kwa sasa umeshaanza katika Jimbo la Chake Chake kwa kule Pemba na Jimbo la Chaani kwa hapa Unguja.

b) Mhe. Spika, serikali inaelewa kwamba ni vizuri kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi nao kuwa na afisi katika majimbo yao kama ambavyo Wabunge wameanza kujengewa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Vile vile tunaelewa kwamba ofisi hizo ni muhimu sana kwa ajili ya kurahisisha kazi za wawakilishi na kuleta ufanisi pamoja na uhusiano mazuri na wapiga kura wao. Lakini kila jambo hutendwa kutegemea na uwezo ulipo. Napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inayo nia ya kujenga afisi hizo kwa ajili ya Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi katika majimbo yao hali itakaporuhusu. Kwa muda huu tunawaomba Waheshimiwa wawe na subira mpaka uwezo wa kufanya hivyo pale utakaporuhusu.

c) Kama nilivyoeleza hapo awali, serikali zetu mbili zinashirikiana kwa karibu katika kuleta maendeleo kwa wananchi wetu. Kwa kuzingatia ukweli huu, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaendelea kushirikiana kwa karibu zaidi na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ili kuleta ufanisi katika suala hili kwa kadiri hali itakavyoruhusu. Ahsante.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri amekiri kwamba hivi sasa wenzetu Wabunge wanajengewa nyumba hizo. Swali.

Kwa kuwa uwezo haujapatikana wa kutosha, lakini wenzetu Wabunge wanajengewa kwa awamu nyumba hizi. Je, serikali haioni haja na sisi ikatujengea kwa awamu?

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, nakubaliana na ushauri wa Mhe. Mwakilishi kwamba kwa kuwa sisi serikali hali yetu ya kuwajengea Waheshimiwa Wawakilishi afisi katika majimbo yao bado haijakuwa nzuri, lakini ushauri wake wa kusema kwamba tuanze na sisi kujenga kwa awamu kama walivyofanya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, basi ushauri huo tumeuchukua, tukijaaliwa tutaufanyia kazi, ahsante.

Mhe. Ame Mati Wadi: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, mimi naomba nitofautiane na Mhe. Waziri kwamba nia ipo. Kama ingekuwa nia ipo, basi tayari ingekuwa Mhe. Waziri keshatengeneza angalau michoro, ili kuonesha kwamba dalili ipo. Lakini mpaka sasa hivi

hakuna makisio wala michoro, wala hajabainisha kwamba lini tunaweza tukaweka vifungu vya ujenzi wa nyumba za Waheshimiwa Wawakilishi.

Kama ipo basi naomba Mhe. Waziri aniambie kwamba angalau lini au mwaka gani tutakabidhiwa michoro ya ujenzi huo wa afisi au nyumba za Waheshimiwa Wawakilishi na kama hazipo Je, ana mpango gani wa kuwashirikisha Wawakilishi na Wabunge ili wakafanya kazi pamoja katika afisi hizo?

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, kama nilivyojibu katika swali la nyongeza la Mhe. Ali Abdalla Ali kwamba serikali baada ya kupata ushauri wa Waheshimiwa Wawakilishi, na mambo mengi Mhe. Spika, serikali inayoyafanya basi mara nyingi mawazo yanatoka katika chombo hiki kitukufu cha Baraza la Wawakilishi.

Kwa hivyo, ndio maana nikasema kwamba kwa kuwa waheshimiwa wameonesha hamu na wao sasa hivi ya kuwa na afisi zao katika majimbo, basi suala hili kama nilivyosema tumelichukua na tukijaaliwa tutalifanyia kazi.

Mhe. Spika, kama alivyosema Mhe. Ame Mati Wadi, jambo ambalo nitaliomba kwa waheshimiwa wale ambao tayari katika majimbo yao yaani hizo afisi kwenye Jimbo la Chake Chake na Jimbo la Chaani, kwa zile afisi ambazo zitakuwa tayari basi tujenge mashirikiano mazuri na ndivyo inavyotakiwa tushirikiane na wabunge wetu ili tuweze kuzitumia afisi hizo kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wetu.

Mhe. Spika, kwa sababu afisi hizi na sivyo kama alivyosema Mhe. Ame Mati Wadi kwamba ni nyumba, hizi ni afisi. Kwa hivyo, afisi kazi yake ni kushughulikia matatizo ya wananchi na kuweza kutafuta namna ya kuyatatua. Pamoja na kwamba huku sisi tunahangaika kutafuta huo uwezo, lakini kwa wale ambao afisi zao zitakazokuwa tayari, basi tunawaomba Waheshimiwa Wabunge na Waheshimiwa Wawakilishi, watumie pamoja afisi hizo na zaidi ukilinganisha kwa hapa Zanzibar, wabunge muda mrefu wanakuwa hawapo Zanzibar, kwa hivyo afisi zitakuwa tupu. Kwa hivyo, ni busara kwamba Waheshimiwa Wawakilishi wakazitumia ipasavyo afisi hizo kwa ajili ya kuleta maendeleo ya wananchi.

Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja: Nakushukuru Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, katika ujenzi wa afisi hizi za wabunge, Jimbo la Koani na Jimbo la Makunduchi nazo zimo.

Mhe. Spika, Mhe. Mbunge na Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Koani walikaa pamoja na waliandaa ramani ya kuongeza chumba kimoja ili Mhe. Mwakilishi apate afisi katika afisi hiyo hiyo ya mbunge. Lakini Mhe. Spika, nasikia bunge wamekataa, nini sababu iliyopelekea Bunge kukataa.

Je, haoni kwamba ipo haja ya Baraza la Wawakilishi na Wabunge viongozi kukaa pamoja wakajadili, ili katika jengo lile ile kuongeza afisi moja ili aweze kupata na mwakilishi itapunguza gharama za ujenzi.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, kwanza suala hili nitamuomba Mhe. Mkuu wa Mkoa nilifanyie kazi kwa karibu zaidi, kwa sababu sijafahamu kwamba labda kuna michoro maalum kwa afisi zote za Bunge. Kama kuna michoro maalum, basi tutaweza kukaa kuzungumza na wenzetu ili kuangalia namna ya kuweza kuboresha hayo mazingira.

Mhe. Spika, kwa sababu unapofanya kitu, zaidi kwa ajili ya waheshimiwa. Nadhani kitu cha msingi zaidi ni kuweza kutoa mawazo yenu na nyinyi kwa kile kitu ambacho mnajengewa.

Kwa mfano, ukilinganisha mazingira ya Bara na ya Zanzibar ni tofauti. Kwa hivyo pengine muundo wa afisi ya Bara au wa Jimbo la Tanzania Bara pengine na muundo wa afisi ya Jimbo kwa Zanzibar hata mazingira yake yanakuwa yako tofauti. Sasa ndio maana nikasema kwamba ni vizuri kukawa na mashirikiano ya karibu baina ya mbunge na mwakilishi ili katika kupanga namna gani ule ujenzi uwepo.

Kwa hivyo, hili tutalifanyia kazi na hata mimi ningependa zaidi afisi hizi zikawa ni ya mbunge na mwakilishi. Kwa sababu viongozi mnapoanza kuwatenganisha, basi na wananchi vile vile tutakuwa tunawatenganisha. Ni busara afisi hizi tukazitumia kwa pamoja.
Mhe. Spika, nitajaribu kuzungumza na wenzetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ili kuangalia uwezekano kama kuna afisi moja, basi kuwe kuna afisi mbili ili waweze kutumia mbunge na mwakilishi.

Vile vile na sisi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na huo uwezo wetu mdogo, tutakuwa tuna nafasi nzuri sasa ya kuingiza hicho kidogo ambacho tulichokuwa nacho kwa ajili ya kujenga hizi afisi zikawa pamoja, ahsante Mhe. Spika.

Nam. 35

Majukumu ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii

Mhe. Ali Abdulla Ali – Aliuliza:-

Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF) ni miongoni mwa majukumu yake ni kukusanya michango ya wanachama (wafanyakazi) kuwalipa wanachama hao mafao ya kustaafu pale wanapostaafu kazi.

(a) Mhe. Waziri tangu kuanzishwa kwake mwaka 2004, ZSSF imeshakuwa na wanachama wangapi.

(b) Kwa kuwa Mfuko huu ni kwa wanachama Je ni wanachama wangapi wameshapewa haki zao.

(c) Je, Mfuko una mpango wa kutoa mikopo kwa wanachama wake.

(d) Kwa kuwa Mfuko huu unajiendesha kibiashara Je, hadi leo ni kiasi gani cha fedha ulichoekeza.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako ninaomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 35 lenye vifungu (a),(b),(c) na (d) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu suali lake Mhe. Mwakilishi, ninaomba kufanya marekebisho madogo kwenye kifungu (a) kuwa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii umeanzishwa kwa Sheria Nam. 2 ya mwaka 1998 na si mwaka 2004 kama ilivyonukuliwa na Mhe. Mjumbe.

(a) Tokea Mfuko wa Hifadhi ya Jamii yaani ZSSF uanzishwe hapa Zanzibar mwezi wa Julai mwaka 1998 na sio mwaka 2004 kama ilivyo kwenye swali la Mhe. Mjumbe, hadi kufikia mwezi Juni, 2009, mfuko umeshasajili wanachama 55,231.

(b) Hadi kufikia mwezi wa Juni 2009, jumla ya wanachama 6,863 wameshalipwa mafao yao ambapo jumla ya T.shs. 6.2 bilioni zimetumiwa kwa malipo hayo.

(c) Mhe. Spika, serikali ina wajibu mkubwa wa kuhakikisha kwamba ukuaji wa *ZSSF* ili iweze kuwa endelevu na kutimiza wajibu wake kwa muda wote. Serikali ilikubaliana na Shirika la Kazi Duniani (*ILO*) kufanya tathmini ya hali na uendelevu wa mfuko. Kwa vile hoja ya mikopo kwa wanachama ni miongoni mwa mambo yaliyozingatiwa katika tathmini ya Mfuko iliyofanywa na shirika la Kazi Duniani (*ILO*), mapendekezo ya ripoti hiyo ikiwemo la mikopo yatawasilishwa serikalini hivi karibuni kwa mazingatio.

(d) Miongoni mwa majukumu ya msingi ya mfuko kama alivyosema Mhe. Mwakilishi, ni kuwekeza kwa nia ya kupata uwezo wa kujiendesha na kulipa mafao.

Mhe. Spikia, hadi kufikia mwezi wa Juni 2009, mfuko tayari ulikuwa umewekeza jumla ya T.shs. 43.97 bilioni katika dhamana za Hazina, akiba za muda maalum yaani *fixed deposit*, na Shs. 18.9 bilioni, kwenye majengo Shs. 4.9 bilioni, ununuzi wa hisa Shs. 2.2 bilioni, vipande vya "*unity Trust of Tanzania*" Shs. 382 milioni na mikopo yenye thamani ya Shs. 112 imetolewa kwa wafanyakazi.

Vile vile *bond* za *Barclays* zenye jumla ya thamani ya Shs. 200 milioni zimenunuliwa. Faida iliyopatikana kwa uwekezaji huo ni Shs. 6.06 bilioni. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo. Mhe. Waziri amekiri kwamba mfuko unawekeza na unapata faida kubwa.

(a) Je. Katika faida hiyo wanachama wake wanafaidika na nini?
(b) Sheria ya kuanzisha mfuko huu imeruhusu watu binafsi wafanyabiashara kuwekeza pia na wao katika akiba zao. Je, Mhe. Spika, anaweza Mhe. Waziri kulijulisha Baraza hili ni watu wangapi mpaka sasa wamewekeza ambao sio wafanyakazi?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, mafanikio makubwa ambayo yameonekana hata kwa wanachama, ni kule kupata mafao yao kwa wakati. Hilo ni suala la msingi kabisa. Mifuko hii kazi yake kubwa ni kuwawezesha kupata mafao yao kwa ule wakati wanapostaafu.

Kwa hivyo, inatokezea kwa mifuko mingine, nafikiri niliwahi kuzungumza. Kuna mifuko ipatayo si chini ya tisa Tanzania. Kwa hivyo, wengine huwa na matatizo, masharti mengi. Lakini mfuko wetu uko moja kwa moja hauna matatizo, ukishafika wakati na yameshawiva mafao yako, basi unalipwa kwa wakati. Nafikiri hiyo ndio faida kubwa ambayo naweza kusema ambayo wanachama wamefaidika.

Mhe. Spika, kuhusu wanachama wangapi ambao wamefaidika na mikopo. Kwa kweli leo nilitoa takwimu nyingi sana ambazo imebidi twende kwenye ma-*file* tukazi-*compile*. Kwa hivyo, sina jawabu sahihi ya *figure*. Lakini Mhe. Spika, tutaifanyia kazi na tumpe *figure* kamili, ahsante.

Mhe. Ame Mati Wadi: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi anayeshughulikia mambo ya Fedha na Uchumi, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, madhumuni ya mfuko ni kuwajengea mazingira mazuri wafanyakazi watakaostaafu. Tangu kuanza kunufaika kwa wafanyakazi ambao wameshastaafu kwa mujibu wa maelezo ya Mhe. Waziri ni karibu watu 6,833.

Mhe. Spika, kadiri siku zinavyokwenda mbele basi wafanyakazi wanaostaafu wanategemea kupata haki zao bila ya usumbufu. Kwa mujibu wa maelezo ya Mhe. Waziri kwamba karibu bilioni 43 mfuko umewekeza na hiki ni kiwango kikubwa sana. Hofu yangu ni kwamba ifikapo mwaka 2020 huenda wakaongezeka maradufu wafanyakazi ambao watastaafu. Hivi haoni Mhe. Waziri bila ya kuangalia vyema uwekezaji wa mfuko huu unaweza kuja kuwasumbua wastaafu. Kama hilo ameliona ni utaratibu gani ambao atawashauri wale wakuu wa mfuko ili wapunguze uwekezaji.

Mhe. Spika, hivi katika uwekezaji huu je, wale wanachama ambao wameshastaafu lakini bado maisha yao ni magumu, Je, upo utaratibu wa kuona kwamba kwa uaminifu wanawakopesha kiasi fulani ili wafanye biashara?

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, naomba kumuhakikishia Mhe. Ame Mati Wadi, pamoja na Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwamba uwekezaji huu wanaofanya Mfuko wetu huu wa Hifadhi ya Jamii usiwatie wasi wasi wowote katika kuwalipa wastaafu au kuwalipa wateja wake wakati utakapofika muafaka.

Kwa sababu Mhe. Spika, utakuta kama nilivyosema tumewekeza katika kununua *share* za Barclays tuna *fixed deposit*, tuna *fixed deposit PBZ*, tuna *fixed deposit* NBC, tuna *fixed deposit FBME* na pia tunanunua *treasure bills BoT*, tuna vipande vya *share* vile nilivyosema *trust fund*. Hii inatuhakikishia

kwamba hizi fedha zetu na sisi zinazunguka. Kwa hivyo, wakati wowote tukizihitajia.

Mhe. Spika, labda katika *fixed deposit* inaweza kuwa kweli tutakwama kwa ule muda uliotakiwa. Lakini watu wetu wametizama au wamepanga muda kwamba baada ya muda tunahakikisha tunapata kiwango fulani cha fedha tena kingi. Wameshapiga mahesabu yao kwamba baada ya mwaka mmoja wanatarajia watu wangapi watastaafu na wanastahiki kiasi gani, baada ya mwaka wa pili kiasi gani.

Mhe. Spika, vile vile tumeshirikiana sana na utumishi na Wizara ya Fedha wanakwenda sambamba, kwa hivyo wasi wasi wowote kwa kweli hakuna. Ni vizuri. Isipokuwa tunaogopa kuwekeza kwenye majengo moja kwa moja, huko tuko-*carefully*. Kwa sababu unajua ukiwa kwenye majengo ukihitajia pesa mpaka uyauze saa ngapi. Lakini kwenye hizi huduma za kibenki nafikiri ni njia nzuri sana wanayoitumia na tuna washauri wazuri na tuna kwenda vizuri Mhe. Ame Mati wala usiwe na wasi wasi.

Mhe. Spika, suala la kupunguza uwekezaji, mimi nafikiri tuwashauri kwamba labda waende vizuri tu, lakini tusiwashauri wapunguze. Hapana. Madhali inatia faida kama nilivyosema tumepata faida ya Shs. 6.6 bilioni sio pesa kidogo hizo. Kwa hivyo, hali ni nzuri na inafaa kwa kweli tuupongeze mfuko wetu unafanya kazi nzuri sana Mhe. Spika.

Mwisho, Mhe. Ame Mati Wadi amesema wakopeshwe wastaafu. Kweli, hiyo ni fikra nzuri. Nafikiri nilipojibu swali la msingi nilisema kwamba tunazingatia sasa mapendekezo ya Shirika la Kazi Duniani (*ILO*) juu ya hili suala zima la mikopo, ikikamilika tutawasilisha serikalini ili tuweze kupata ruhusa ya kulitekeleza, ahsante Mhe. Spika.

Nam. 72

Ujenzi wa Nyumba za Makaazi Karibu na Visima Vya Maji

Mhe. Ali Denge Makame - Alijibu:-

Kwa kuwa maji safi na salama ni muhimu sana kwa afya zetu na kama inavyoeleweka wazi kwamba maji hayo pia ni muhimu kwa ustawi wa viumbe mbali mbali.

(a) Je, Mhe. Waziri kuna mita ngapi baina ya kisima cha “Borehole” na makaazi ya wananchi ili wananchi hawa wasiharibu mazingira kwa kuchimba vyoo karibu na kisima hicho.

(b) Mhe. Waziri je, wizara yako ina mpango gani kwa wale wote waliojenga nyumba karibu na visima hivyo na chem chem nyengine za maji.

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 72 lenye kifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, wengi wetu tunaamini kwamba uchafuzi wa vyanzo vya maji vikiweno visima, chemchem, mito, mapango ya maji, unasababishwa na vyoo vya majumbani tu, ukweli ni kwamba uchafuzi huo unatokana na sababu tofauti, zikiwemo takataka za mchanganyiko zenye kuvujisha sumu (*leaching field*) kama mbolea, madawa ya kuuliya wadudu, maji machafu yanayotoka viwandani, mafuta na vilainisho vya magari na kadhalika.

Mhe. Spika, shughuli nyengine zinazosababisha uchafuzi wa vyanzo vya maji ni makaazi ya watu, makaburi, vyoo na harakati nyengine za binaadamu. Baada ya maelezo yao, sasa nimjibu kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, kwa mujibu wa kanuni za maji ya mwaka 2007 kifungu cha 5 na 6 kinaeleza umbali wa kisima cha "*borehole*" na makaazi ya watu kunahitajika umbali wa angalau mita 500 kwa maeneo ya chini ya chanzo cha maji (*downstream*). Aidha, masafa baina ya kisima na vyoo kunahitajika umbali wa angalau mita 75.

Mhe. Spika, kwa taarifa za nyongeza masafa yanayohitajika baina ya takataka za mchanganyiko zenye kuvujisha sumu (*leaching field*) ni angalau mita 500 na baina ya visima na makaburi ni angalau mita 50.

Mhe. Spika, hata hivyo masafa haya yanatakiwa kuzidi kulingana na ukubwa wa eneo la vyanzo vya maji, aina ya miamba (*geological formation*) na aina miziamo (*drainage*) iliopo katika eneo hilo.

(b) Mhe. Spika, Wizara yangu tayari imeshachukua juhudi tafauti ikiwemo ya kutoa matangazo (*declarations*) la uhifadhi wa maeneo maalum ya maji kitaifa katika maeneo mbali mbalimbali ya vyanzo vya maji kuwa na maeneo maalum ya vyanzo vya maji (*catchment areas*).

Mhe. Spika, kutangazwa kwa maeneo hayo ni kielelezo wazi kuwa Wizara imechukua jitihada za kuvitunza vyanzo hivyo. Hatua zinazoendelea

kuchukuliwa na Wizara yangu ni kupima maeneo hayo kwa nia ama ya kuyaainisha kwa mipaka maalum au kuwa milikisha Mamlaka ya maji kwa nia ya kuwadhibiti watumiaji wengine wa maeneo hayo kuyatumia visivyo.

Mhe. Spika, hatua muwafaka zinazohitajika kwa wale wote waliojenga nyumba karibu na visima, chemchem na vyanzo vyengine vya maji ni pana kiasi ambacho kunahitaji umakini katika kulishughulikia, kwani sasa limegeuka na kuchukua sura ya kitaifa.

Mhe. Spika, kwa hivyo nalishauri Baraza lako Tukufu pamoja na mihimili mingine ya nchi kuwa karibu na kuisaidia Wizara yangu katika azma yake ya kulinda na kuendeleza rasilimali hii muhimu kwa Taifa na wananchi wake.

Mhe. Ali Denge Makame: Mhe. Spika, ahsante pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri kwa kujibu kwa ufasaha, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Katika majibu yake ameeleza kuhusu visima vya *borehole* pamoja na zile chemchem za maji kujenga makaazi ya wananchi, ambao nyumba zao zina visima vya kina kirefu ni masafa ya mita mia tatu ndio ajenge nyumba yake.

Je, kwa wale ambao hivi sasa majengo yapo karibu na visima hivyo ambao hawakufikia urefu wa mita mia tatu, anachukua hatua gani za kuwahamisha au kuwalipa fidia kwa ajili ya kwenda kuhamia sehemu nyengine?

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, ni kweli kuna watu wamejenga nyumba zao karibu na vyanzo vya maji ambapo hayafikii yale mafasa yanayotakiwa. Kwa hivyo, ni vyema maeneo haya yasiwe na nyumba na hata wale ambao wamejenga basi tukawahamisha, lakini kwa hivi sasa hatuna mpango huo. Isipokuwa kinachotusaidia kwa hapa Zanzibar bahati nzuri visima vyetu vingi vina kina kirefu. Kutokana na hali hiyo, ile athari ya maji yetu kupata ile *contamination* kidogo inakuwa inapungua.

Kwa hivyo, nadhani Mhe. Mwakilishi pamoja na wananchi kwa jumla wasiwe na wasi wasi sana kuhusiana na hali hii. Kwa kweli inachosaidia ni kwamba visima vyetu vina kina kirefu kuanzia mita 45 na kuendelea, lakini kama vingekuwa vya mita 10 unapata yale maji ya uhakika, basi hali ingekuwa mbaya sana.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa ruhusa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali.

Katika jibu la swali mama alisema kwamba utaratibu wa kuchimba kisima baina ya nyumba na kilipo kisima pana mita maalum. Lakini alisema kwamba wananchi wetu wengi sana bado wanachimba kinyume na taratibu hizo. Je, kama Wizara inaweka mikakati gani ya kuweza kuwafahamisha wananchi hao, ili kuepukana na tatizo hilo?

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, wakati nilipokuwa nikijibu swali mama nilisema, hivi sasa Mamlaka ya Maji kwanza inatoa taaluma hiyo kwa wananchi juu ya ujenzi wa nyumba zao kuwa zisiwe karibu na vyanzo vya maji. Vile vile tumefanya utaratibu wa kuyapima maeneo yale pamoja na kuyawekea mipaka, ili kuondoa hilo tatizo la uvamiji wa makaazi kwa watu wengine.

Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja: Mhe. Spika, nashukuru na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kweli tunajua kwamba nyumba za Mji Mkongwe zimekamatana kama meno, lakini kuna visima vingi ambavyo vimechimbwa. Je, Wizara imefanya uchunguzi maji yake kwenye visima vile yako kama yako salama?

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Spika, ni kweli maeneo si ya Mji Mkongwe tu, yaani maeneo mengi hata ya Ng'ambo watu ndani ya nyumba zao wamechimba visima. Lakini sehemu kubwa ya matumizi ya maji yake hasa wanayatumia kwa shughuli nyengine na wala si za kunywa, kama vile kwenye kufulia na kuoshea. Kwa hivyo, ikiwa hakuna budi kuyatumia kwa masuala ya kunywa basi huwa wanayachemsha, kwa sababu maji yale hayana salama sana.

Kwa kweli kama nilivyosema kwamba vile visima vilivyochimbwa ni virefu sana. Hivyo, ile *contamination* ya maji yale na vyoo inakuwa hatari yake si kubwa sana, lakini yale maji hayana salama sana.

Nam. 21

Malipo kwa Walioumia Mikarafuuni

Mhe. Ali Abdalla Ali – Aliuliza:-

Maagizo na ushauri uliotolewa na Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi kwa mwaka wa fedha 2008/2009 ni kuwalipa watu 355 walioumia mikarafuu tangu mwaka 2002. Idara ya Ustawi wa Jamii imeshakamilisha hatua za utengenezaji wa malipo kilichobaki ni Wizara kupitia Shirika la *ZSTC* kutoa malipo hayo.

(a) Je, Mhe. Waziri suala hili unalikumbuka?

(b) Kwa kuwa kazi zote za awali kisheria zimekamilika. Je, watu hao 355 watalipwa lini fedha zao?

(c) Je, Mhe. Waziri ni kiasi gani cha fedha kwa ujumla wake watalipwa watu hao?

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara, Uwekezaji – Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 21 kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Tatizo la watu 355 walioanguka mikarafuu na ambao bado hawajalipwa fidia na Shirika la *ZSTC* linafahamika na Wizara yangu. Hata hivyo, kama nilivyojibu wakati wa mjadala wa bajeti ya Wizara yangu, kwamba hivi sasa Shirika halina uwezo wa kulipa fidia kwa walioanguka mikarafuu kutokana na hali mbaya ya kifedha.

Mhe. Ame Mati Wadi: Mhe. Spika, ahsante pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Hivi sasa waliogusiwa ni watu hawa 355 ni sehemu ya miaka hiyo iliyotajwa, lakini kuna watu wengi ambao walioanguka mikarafuu bado hawajalipwa. Kwa kweli siku zote maelezo wanayoyapata ni haya, yaani watu wanajenga matumaini wanaanguka mikarafuu na wala hawapati fidia.

Mhe. Spika, nafahamu kwamba Shirika la Biashara la *ZSTC* hivi sasa halina fedha, lakini upo utaratibu wa Serikali wakiona kwamba jambo linahusu Serikali na shirika halina fedha wanatafuta utaratibu. Kwa mfano, kulikuwa na Shirika la Bizanje, Songambele na watu walipatiwa haki zao na kulipwa, yaani Serikali ilitenga fedha.

Hivyo, Wizara ya Utalii, Biashra na Uwekezaji imeishauri Wizara ya Fedha na Uchumi kuhusiana na suala hili? Mhe. Spika, kama uwezekano haupo kwa huko mbele tunakokwenda, basi ni bora zaidi tukawapa ukweli wananchi wakati wanapoanguka mikarafuu hakuna fidia.

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Spika, Wizara yangu mara kadhaa imekuwa ikifanyakazi ya kutafuta fedha kwa ajili ya Shirika la *ZSTC* pamoja na Wizara ya Fedha na Uchumi, lakini bado hatujafanikiwa. Kwa hiyo, kama nilivyosema kwamba shirika litakuwa kwenye hali nzuri kifedha, basi walioanguka watapatiwa malipo yao. Isipokuwa kama kutakuwa na mambo au maamuzi mengine ya kiserikali basi taarifa itatolewa.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji, naomba kuongezea kwamba tumechukua *concern* yake Mhe. Mwakilishi na tutashirikiana pamoja na Mhe. Waziri wa Wizara husika, kwa ajili ya kukaa pamoja kama Serikali ili tuweze kuona tunalikwamua vipi tatizo hili na kuweza kuondoa hiki kilio cha hawa wananchi walioathirika *(Makofi)*.

Nam. 6

Kufunguliwa Hoteli katika Mwezi wa Ramadhani

Mhe. Ame Ussi Juma – Aliuliza:-

Tunaipongeza Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuheshimu uhuru wa kuabudu kwa wananchi wake, ikiwa ni pamoja na kupiga marufuku uuzwaji wa chakula na kula hadharani wakati wa mchana wa mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Serikali inachukuwa hatua hizi kwa lengo la kudumisha amani na utulivu miongoni mwa waumini wa Dini ya Kiislamu na kuimarisha uvumilivu wa dini kwa wasiokuwa wafuasi wa Dini ya Kiislamu.

(a) Mhe. Waziri, je unafahamu kwamba baadhi ya Mikahawa na Mahoteli ya Kitalii, inakuwa wazi na kuuza chakula wakati wa mchana wa mwezi wa Ramadhani?

(b) Je, Wizara yako inachukua jitihada zipi kwa wamiliki wa Mahoteli ya Kitalii, kuhakikisha kwamba haziuzi chakula wakati wa mchana wa mwezi wa Ramadhani?

(c) Kwa kuwa kuna baadhi ya mikahawa na mahoteli maeneo ya Mji Mkongwe huwa wazi wakati wa mchana wa mwezi wa Ramadhani. Je, Wizara imechukua hatua zipi dhidi ya wamiliki wa mikahawa na hoteli hizi?

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji – Alijibu:-

Mhe. Spika kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 6 lenye kifungu (a), (b), na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, ni kweli kwamba hoteli za kitalii na mikahawa ambayo ni sehemu ya hoteli za kitalii, huwa inakuwa wazi kutoka huduma za chakula na vinywaji wakati wa mchana ndani ya mwezi wa Ramadhani. Wizara imeweka utaratibu huu kwa masharti kwamba

lazima shughuli hizi zifanywe ndani ya Hoteli na Mikahawa hiyo, kwani wengi wa wageni wanaofikia katika hoteli hizo huwa sio waislamu na sio busara kuwanyima huduma hiyo.

Hata hivyo, Wizara yangu haina taarifa kama baadhi ya mikahawa ambayo sio sehemu ya Hoteli za Kitalii huwa wazi na kuuza chakula wakati wa mchana wa mwezi wa Ramadhani. Tutashukuru sana kama tutashirikiana pamoja siku za usoni kwa Serikali kupatiwa taarifa hizo kwa ajili ya kuchukua hatua zinazofaa.

(b) Kama nilivyotangulia kusema kwamba watalii wanaotembelea nchi yetu ni wenye dini mbali mbali. Hata hivyo, Wizara yangu inachukua hatua zifuatazo:-

i. Inapokaribia tu mwezi wa Ramadhani hutoa miongozo/agizo kwamba mikahawa yote ambayo sio sehemu ya Hoteli za Kitalii inatakiwa ifungwe na isitoe huduma yoyote wakati wa mchana.

ii. Hoteli zote za kitalii na mikahawa ambayo ni sehemu ya hoteli ya kitalii lazima watowe huduma za chakula na vinywaji ndani ya hoteli na mikahawa hiyo.

iii. Kuwataka watembezaji wageni kuwashauri wateja wao kutofanya mambo ambayo ni kinyume na silka na utamaduni wa Kizanzibar kufanywa hadharani na hasa wakati wa mwezi wa Ramadhani. Baadhi ya mambo yao ni kama kula, kunywa, kuvuta sigara na kadhalika.

(c) Wizara inayo taarifa ya hoteli na mikahawa ambayo ipo ndani ya Wizara yangu na iliyoruhusiwa kutowa huduma kwa watalii tu. Aidha, kuhusu hoteli zisizokuwa chini ya usimamizi wa Kamisheni ya Utalii, Wizara yangu iko tayari kutoa ushirikiano kwa mamlaka husika, ili kuzuia uzwaji wa chakula kiholela katika mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Mhe. Haji Mkema Haji: Mhe. Spika, baada ya majibu ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mjumbe aliyeuliza swali alikuwa na mantiki ya kwamba Sera yetu ya Masuala ya Ajira za Mikawaha shughuli hii iendeshwe na Wazalendo. Kwa hivyo, tatizo liliopo kwa baadhi ya mikahawa kuachiwa wageni kufanya biashara hiyo na wao masuala ya mwezi Mtukufu wa Ramadhani hawafahamu ambayo ni kinyume na silka zetu.

Mhe. Spika, hivi Mhe. Waziri nakumbuka kwa Khamis Machungwa upo mkahawa unaoitwa *Latavan*, ambao ulikuwa ukiuza chakula mchana na ukiendeshwa na mgeni.

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Spika, nakumbuka tena ninajua kwamba Mkunazini upo Mkahawa unaoitwa *Latavan* na unaendeshwa na mgeni.

Nam. 38

Uchakavu wa Viwanja vya Kufurahishia Watoto

Mhe. Ali Abdulla Ali – Aliuliza:-

Baada ya Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964, Rais wa kwanza wa Zanzibar, Marehemu Mzee Abeid Amani Karume miongoni mwa maendeleo aliyoyaleta ni kujenga viwanja vya kufurahishia watoto, Kariakoo Unguja na Tibirinzi Pemba. Hata hivyo, viwanja hivyo kwa sasa ni vibovu, bado havijafanyiwa matengenezo yoyote na kupelekea kuhatarisha usalama wa watoto wetu.

(a) Je, Mhe. Waziri tulisikia kuwa viwanja hivyo vimepata mdau wa kuvifanyia matengenezo ni kweli?

(b) Mdau huyo ni nani, kazi ya kuvifanyia matengenezo itaanza lini na kwa gharama za kiasi gain?

(c) Kwa kuwa hivi sasa hali ya viwanja hivi inazidi kuwa mbaya. Je, Wizara ina mpango wowote wa kuvihami, ili visiendelee kuhabirika?

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako swali lake Nam. 38 lenye kifungu (a), (b), na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza kabla sijamjibu Mhe. Mwakilishi naomba nikiri kweli kwamba viwanja vya kufurahishia watoto, Kariakoo Unguja na Tibirinzi Pemba, kwa hivi sasa bado havijafanyiwa matengenezo yoyote.

(a) Ni kweli kuwa viwanja vya kufurahishiwa watoto vya Tibirinzi Pemba na Kariakoo Unguja vimekabidhiwa kwa mdau, ambayo ni Taasisi ya Serikali ijulikanayo kwa jina la Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*ZSSF)*, kwa ajili ya kuviendeleza pamoja na kuvifanyia matengenezo.

(b) Kwa vile tayari Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo imeshaikabidhisha viwanja hivyo kwa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*ZSSF*) hapa Zanzibar. Gharama halisi za matengenezo na lini kazi hiyo itaanza, Wizara yetu haihusiki moja kwa moja, kwani hilo limo kwenye Mamlaka ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, baada ya makabidhiano hayo rasmi kufanyika.

Isipokuwa tunachokifahamu kupitia vyombo vya habari ni matangazo ya kutafuta Mshauri Mwelekezi tayari yameshatoka na mchakato wa kumpata huyo atayeshughulikia umeanza.

(c) Mhe. Spika, ni kweli kuwa hivi sasa hali ya viwanja inazidi kuwa mbaya, ndipo Serikali ilipochukua uamuzi na hatua za dharura za kuipa Taasisi ya Serikali (*ZSSF*) ili kuvihami viwanja hivyo. Kwa taarifa tu *ZSSF* ilivifanyia matengenezo madogo viwanja hivi na vimeweza kutumika katika Siku Kuu ya Idd El Fitri tu.

Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja: Mhe. Spika, nashukuru na mimi kunipa nafasi, ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Katika jibu mama Mhe. Naibu Waziri ametueleza kwamba viwanja hivi wamepewa *ZSSF*, lakini viwanja hivi wakati vilipojengwa viliwekwa mageti na vijana wanapokwenda pale wakitozwa malipo ya geti.

Mhe. Spika, kwenye miaka ya 1980 watoto ndani ya kiwanja cha Kariakoo walitishana nyoka na wote walikwenda mbio na kufukuzia kwenye geti na matokeo yake watoto wawili walifariki na wengi wengi kujeruhiwa.

Sasa baada ya kupewa *ZSSF* wamerudisha tena utaratibu wa kuweka mageti na kutoza malipo ya geti. Swali langu je itakapotokea kama yale yaliyotokea miaka ya 1980 haoni itakuwa na mashaka makubwa pale? Kwa hivyo, anaishauri nini *ZSSF* kwa ajili ya kuweka usalama yasijekutokea kama yaliyotokea mwaka ule?

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, kwanza uamuzi wa kuipa Mfuko wa Hifadhi ya jamii (*ZSSF*) kiwanja hicho ulifanyika kwa sababu ni kiwanja ambacho kinahusu jamii moja kwa moja. Kwa sababu angepewa mtu binafsi pengine angeweza kutoza fedha nyingi zaidi wakati wa kiingilio na watu wasingeweza kuwa na kulipa fedha hizo, hilo limefanyika kwa sababu hiyo.

Kwa kweli hivi sasa ajali kama hiyo haiwezi kutokea kwani mageti yote yanatumika ya kiwanja hicho. Kwa mfano, geti lilioko mbele, upande wa kulia

wa kiwanja, upande wa barabara kuu kulia pamoja na sehemu ya nyumba karibu na ile *Taxe Stand*. Kwa hivyo, ajali ya namna kama hiyo hivi sasa hakuna wasi wasi wa kutokezea, kwa sababu kuna njia za kutosha za kuingia na kutoka kwenye kiwanja hicho na wakati wa Siku Kuu mageti yote huwa yanafunguliwa.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri. Katika jibu lake mama amekiri kwamba viwanja hivyo ni vibovu, lakini alisema kwamba vimefanyiwa ukarabati kidogo na katika Siku Kuu hii iliyopita vijana walikwenda kufurahika.

(a) Je, mapato ya kiwanja hicho kwa hivi sasa anakusanya mwenyewe mwekezaji au Wizara?

(b) Kwa kuwa hivi sasa kinajikongoja kuna maduka ya wafanyabiashara kama vile *chips* na kadhalika. Je, pato hilo linakwenda kwa nini?

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, kwanza naomba nimpongeze kwa swali zuri sana alilouliza, ambalo naamini litaweza kutuelimisha sote kwa pamoja na linanisaidia mimi kwa sababu hivi karibuni nilitembelea hivyo viwanja na kuweza kuyajua yote hayo.

Kwanza kabisa wakati wa Sikukuu yalifanywa matengenezo madogo kwa baadhi ya mashine kutiwa vifaa vipya pamoja na kuwekewa *greece* na kama tutakumbuka lile pembea kubwa na hata zile za farasi na *train*, basi ziliweza kufanyakazi na watoto waliweza kufaidika.

Kwa hivyo, mapato yake yote yalikusanywa na wenyewe *ZSSF*, kwa sababu wakati huu tayari walikuwa wameshakabidhiwa na wale wafanyakazi ambao wako pale wako chini ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii moja kwa moja hata upande wa mishahara wanayolipa ni wenyewe *ZSSF*. Kweli kuna mapato mengine yanayotokana na maduka pamoja na afisi mbali mbali ambazo zimo ndani ya kiwanja kile.

Lakini tunachofahamu walichofanya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa ajili ya yale matengenezo makubwa, tayari wameshaandika barua, ili wamalize ile mikataba yao na waweze kuhama kwa ajili ya kufanyika matengenezo makubwa ya kiwanja kizima cha kufurahishia watoto *(Makofi)*.

Mhe. Ame Mati Wadi: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja dogo, kwa sababu nina wasi wasi. Wakati Mhe. Naibu Waziri alipokuwa akijibu alisema kwamba matayarisho ya

matengenezo ya kiwanja hiki hawayajui gharama zake, kwa sababu tayari wameshawapa *ZSSF*.

Mhe. Spika, hofu yangu ni kwamba unapotaka kubadilisha au kutoa kitu, yaani mtaji wa umma kuna sheria maalum inayoitwa Sheria ya Mitaji ya Umma, inavyoonekana hivi sasa kwamba taasisi hii inaondoka kwake na kwenda kwenye taasisi nyengine ya Serikali.

Hivyo, Mhe. Waziri haoni kufanya hivyo ni kosa kubwa sana na kama amewapa *ZSSF*, amewapa kwa sheria gain? Hata hivyo, haiwezekani Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo iwe haina chake, hivyo Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo katika hali hiyo itakapokuwa tija ipo wao watafaidika kiasi gani?

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, ninavyofahamu mimi kwa upeo wangu, Serikali inaweza kufanya maamuzi ndani ya taasisi zake, kufanya mabadiliko ya taasisi moja ya Wizara kwenda katika Wizara yoyote nyengine na Serikali inao uwezo huo.

Maamuzi hayo rasmi yalipitishwa na Kikao rasmi cha Baraza la Mapinduzi (BLM) kuikabidhisha taasisi hiyo, yaani Viwanja vya Kufurahishia Watoto Kariakoo na Tibirinzi kukabidhishwa kwa *ZSSF* na Serikali inayo mamlaka hayo kamili ya kuweza kufanya hivyo. Mhe. Spika, ahsante sana.

Nam. 43

Misaada ya Fedha kutoka kwa Wadau wa Michezo

Mhe. Ali Abdulla Ali – Aliuliza:-

Muda mrefu Chama cha Mpira wa Miguu cha Zanzibar (*ZFA*) na kile cha Tanzania Bara (*TFF*) vilikuwa na malumbano katika masuala mbali mbali ya kimichezo. Miongoni mwa masuala yanayolalamikiwa ni kuwa fedha za misaada kutoka kwa Washirika mbali mbali wa Maendeleo wakiwemo *FIFA* zinatumiwa upande mmoja tu wa Tanzania (Tanzania Bara).

(a) Je, Mhe. Waziri suala hili unalifahamu?

(b) Kwa kuwa mambo mengi ya nje Zanzibar inatumia mwamvuli wa Tanzania. Je, ni kiasi gani cha fedha imepatiwa Zanzibar kutoka *FIFA*?

(c) Kwa kuwa Mhe. Waziri ulituahidi kuwa utakaa na Waziri wa Tanzania Bara, ili kutatua tatizo hili. Je, suala hili limefikia hatua gani?

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 43 lenye kifungu (a), (b), na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli kuwa Chama cha Mpira wa Miguu Zanzibar (*ZFA*) na kile cha Tanzania Bara (*TFF*) vilikuwa na malumbano katika masuala mbali mbali ya kimichezo kwa muda mrefu.

Mhe. Spika, naomba wakati najibu swali hili waandishi wa habari wanisikilize vizuri, kwa sababu jana walini-*misquote* kwenye tathmini iliyotoka katika Redio Jamii ya Micheweni, waliandika idadi ya fedha ambayo siyo niliyoitaja hapa. Kwa hivyo, naomba kwa suala hili nisikilizwe vizuri, ili niweze kueleweka.

(a) Suala hili la malumbano kati ya *ZFA* na *TFF* tunalifahamu na kwa kiasi kikubwa hivi sasa limeshatatuliwa kupitia vikao mbali mbali vilivyofanywa kwa kuzikutanisha pande zote mbili zinazolumbana, yaani *ZFA* na *TFF*. Vikao hivyo, vilifanywa chini ya usimamizi wa Mabaraza mawili, yaani Baraza la Michezo na Zanzibar na lile la Tanzania.

Baada ya hapo vikao hivyo *ZFA* na *TFF* pamoja na Mabaraza mawili ya Michezo zilikuwa pamoja na Wizara mbili za pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano Tanzania, yaani Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kutoka Tanzania Bara pamoja na Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo ya hapa Zanzibar.

(b) Kwa kuwa Zanzibar kwenye masuala ya nje inatumia mwamvuli wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pande mbili hizi tayari zimeshakaa pamoja na kuainisha maeneo mbali mbali yenye mapungufu na yanayohitaji ushirikiano kama vile maeneo yanayohusiana na misaada inayotoka moja kwa moja nje, kwa ajili ya mpira wa miguu pamoja na ile inayotoka *FIFA*, mafunzo, ushiriki wa Timu zetu kwenye Mashindano ya Kimataifa.

Vile vile katika ushiriki wa Mikutano Mikuu ya *FIFA* pamoja na Mikutano ya Viongozi wa Vyama vya Mpira wa Miguu, ambao

hufanyika huko Makao Makuu ya *FIFA* nchini *Geneva Uswiss* pia likiwemo suala la *FIFA*.

(c) Mhe. Spika, naomba nimfahamishe Mhe. Mwakilishi kwamba ile ahadi tayari imetimizwa ile iliyotolewa na Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo hapa ndani ya Baraza lako tukufu la Wawakilishi.

Hivyo, Wizara yetu ya Habari, Utamaduni na Michezo tayari imeshakutana na kukaa pamoja na Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania pamoja na mawaziri wawili akiwemo Mhe. Ali Juma Shamuhuna kutoka hapa Zanzibar na Mhe. George Huruma Mkuchika kutoka Tanzania Bara na kufikia maamuzi muafaka katika kuyapatia ufumbuzi masuala mbali mbali ambayo yalijitokeza na wala sio yale ya mpira wa miguu tu, bali na masuala mengine ambayo yalikuwa ni kero kwa vyama vyetu vya michezo vya pande mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Spika, kilichobaki sasa ni utekelezaji kwa watendaji kwa yale yote yaliyokubaliwa na mawaziri wa pande zote mbili ambao walishirikishwa hao watendaji wenyewe.

Nam. 12

Uanzishwaji wa Baa Kiholela katika Makaazi ya Wananchi

Mhe. Ame Ussi Juma – Aliuliza:-

Pombe za namna yoyote ikiwa ni gongo, bia ama madawa ya kulevya na nyenginezo ni kinyume na utamaduni wa Mzanzibari. Kwa kuzingatia ukweli huu, kitendo cha kuanzisha baa na zaidi maeneo ya makaazi ya wananchi, sio tu kinyume na utamaduni wetu tuliourithi kutoka kwa wazazi wetu, lakini ni kusababisha uhalifu mbali mbali.

(a) Je. Mhe. Waziri unafahamu kuwa hivi sasa baa nyingi zimeanzishwa katika makaazi ya wananchi?

(b) Je, utakubaliana na mimi kwamba, hatua hii ya baa ndani ya mitaa yetu imechangia sana kuiharibu Zanzibar kimaadili na kuongeza wimbi la uhalifu?

(c) Kwa kuzingatia ukweli huu. Je, utakubaliana na mimi kwamba sasa umefika muda wa kuzitokomeza baa hizi, ili kuilinda Zanzibar na wananchi wake kimaadili na kiutamaduni.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya S.M.Z – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 12 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali haifahamu kuwa hivi sasa baa nyingi zimeanzishwa katika makaazi ya Wananchi. Ninachofahamu ni kuwa baa nyingi zimefungwa baada ya wananchi kupinga kuwepo kwa baa hizo katika maeneo yao. Jumla ya baa 12 katika Wilaya 6 za Unguja zimefungwa kuendesha biashara hiyo.

(b) Kuanzishwa kwa biashara ya baa ndani ya mitaa yetu, kunaweza kuwa kiashiria kimoja wapo cha kuharibika kwa maadili ya Mzanzibari na kuongezeka kwa wimbi la uhalifu. Ndio maana katika Sheria ya Vileo wananchi wamepewa fursa ya kupinga kuanzishwa kwa biashara hiyo katika maeneo yao.

(c) Napenda ifahamike kuwa biashara ya baa inafanywa kwa mujibu wa Sheria na kwamba wenye kuendesha biashara hiyo wanapewa leseni halali. Ili kuitokomeza kabisa biashara hiyo, kwanza Serikali italazimika kuifuta Sheria hiyo. Vile vile Serikali itakuwa tayari kufanya hivyo pindi ikiona ipo haja hiyo kwa faida ya wananchi wake.

nam. 48

Matengenezo ya Uwanja wa Ndege wa Kimataifa Zanzibar

Mhe. Ali Abdulla Ali – Aliuliza:-

Naipongeza Serikali kupitia Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kwa matengenezo makubwa ya Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Zanzibar katika eneo la njia ya kurukia ndege, ili ndege kubwa ziweze kuruka na kutua bila ya matatizo. Kazi hii inafanywa na Kampuni ya *Mecco* na imeshafikia hatua nzuri ya matengenezo.

(a) Mhe. Waziri kwa kuwa tatizo la uwanja wetu sio njia ya kurukia ndege tu, lakini eneo la kufikia wageni na kuondoka unahitaji matengenezo. Je, eneo hili limewekewa mkakati gani?

(b) Sehemu ya *Parking* ya ndege kubwa hili pia ni tatizo. Je, Wizara ina mkakati gani juu ya suala hilo?

(c) Je, matengenezo ya eneo la njia za kurukia ndege imegharimu kiasi gani cha fedha?

Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi – Alijibu**:-**
Mhe. Spika kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe Mwakilishi swali lake Nam. 48 lenye kifungu (a), na (b) kama ifuatavyo:

a) Nakubaliana na maelezo ya Mhe. Mwakilishi kuwa tatizo la uwanja wetu au mahitaji ya uwanja wetu sio njia ya kurukia na kutulia ndege tu, lakini pia eneo la kufikia wageni na kuondokea (jengo la abiria) ambalo linahitaji mategenezo makubwa. Hata hivyo, wizara yangu imeandaa mkakati wa kukifanyia matengenezo makubwa Kiwanja cha Ndege cha Zanzibar ikiwemo utanuzi wa jengo la abiria ambalo umeanza kutekelezwa, ambapo kazi za usanifu na utayarishaji wa michoro pamoja na mahitaji ya gharama zake zimekamilika. Hatua inayofuata ni utekelezaji wa kazi hiyo kifedha ambapo mchango wa serikali ni shilingi milioni mia sita unahitajika na sehemu iliyobakia itatolewa na mfadhili wa ujenzi huo. Katika mpango wa muda mrefu serikali inakusudia kujenga jengo jipya la abiria katika Kiwanja cha Ndege cha Zanzibar.

b) Kwa upande wa eneo la kuegeshea ndege wizara yangu inakusudia kufanya utanuzi katika eneo hilo ili liweze kumudu kuegesha ndege kubwa zaidi kwa wakati mmoja, sambamba na ujenzi wa jengo jipya la abiria ambao unaendana pamoja na ujenzi wa maegesho hayo ya ndege.

c) Gharama za matengenezo ya barabara ya kurukia na kutulia ndege ni shilingi 42,591,362,189. na matengenezo hayo yanafanywa na Kampuni ya Sogea-Satom ya Ufaransa na sio Kampuni ya Mecco kama alivyoeleza Mhe. Mwakilishi katika swali lake.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Mhe. Waziri kila bajeti anayosema suala la uzio limo katika mpango na kutokuwepo kwa uzio katika kiwanja chetu kunahatarisha usalama wa ndege zinazotua na zinazoruka.

Je, ni lini kutazungushwa uzio kiwanja chetu au tunangoja miaka mitano imalizike.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, ni kweli kwamba katika moja ya mambo ambayo serikali inayapa kipaumbele kwa viwanja vyetu vyote viwili ni ujenzi wa uzio, na kwa makisio ambayo yamefanywa awali ni kwamba Uwanja wa Ndege wa Zanzibar zinatakiwa karibu bilioni tano kwa ajili ya uzio. Kwa hivyo, huu ujenzi wa njia ya kurukia na kutua ndege unafadhiliwa na *World Bank* ili wakubali tuendelee na ujenzi wa uzio ili kurahisisha kazi katika eneo la uwanja wetu wa kimataifa. Lakini kwa upande wa Pemba kama nilivyozungumza juzi kwamba serikali imeamua kuwa itaanza wenyewe kujenga uzio kwa Pemba huku ikifuatilia mkopo kutoka *ADB* ili tuweze kujenga uzio kunusuru hali za viwanja vya ndege ambapo haviruhusiwi kutokuwa na uzio viwanja vyetu.

Nam. 57

Usafirishaji wa Mazao ya Matunda

Mhe. Ali Abdulla Ali - Aliuliza**:-**

Kisiwa cha Pemba kinasifika kwa kuzalisha ndizi za aina mbali mbali hasa katika mwezi Mtukufu wa Ramadhani pamoja na matunda kama vile embe na mabungo. Baadhi ya bidhaa hizo hutumiwa na wakulima wenyewe na ziada zikasafirishwa na kuletwa Kisiwa cha Unguja na kwengineko kwa kuuzwa.

(a) Mhe. Waziri, bidhaa zote zinatoka nje ya nchi huwekewa takwimu. Je, bidhaa kutoka Pemba kuja Unguja nazo pia hufanyiwa hivyo.
(b) Kama ndio, Je, kuanzia mwezi Januari 2009 hadi Septemba 2009 ni tani ngapi za ndizi zililetwa Unguja kibiashara.
(c) Zina thamani ya kiasi gani cha fedha.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira - Alijibu**:-**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 57 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, ni kweli bidhaa zote zinatoka nje ya nchi huwekewa takwimu, ikiwa ni pamoja na bidhaa kutoka Pemba kuja Unguja nazo pia hufanyiwa hivyo.

(b) Mhe. Spika, kuanzia mwezi wa Januari, 2009 hadi Septemba, 2009 jumla ya kilo 1,199,500 sawa na tani 1,199.5 za ndizi za aina mbali mbali zimeingizwa Unguja kutoka Pemba.

(c) Mhe. Spika, kulingana na wastani wa bei zilivyokuwa katika vipindi tofauti katika soko kuu la Unguja ndizi zilizoingizwa zilikuwa na thamani ya Tsh. 719,700,000.00.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri amekiri kwamba takwimu za bidhaa zote kutoka nje hata Pemba na Unguja huwa zinawekwa, lakini hivi sasa Pemba sio ndizi tu na mabungo hata samaki na pweza wanaletwa kutoka Pemba kuja kuuzwa hapa Unguja.
Je, hilo ni kweli na takwimu hizo anazo.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Spika, nataka nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba bidhaa zote zinazoingizwa kutoka Pemba zinafanyiwa takwimu yake. Halafu nataka nimwambie Mhe. Mwakilishi kwamba suala hili tutamletea kwa maandishi na sio samaki peke yake wanaoletwa hapa Unguja kuna pweza, kuku na hata chaza pia wanaletwa.

KUAKHIRISHWA BARAZA KABLA YA WAKATI WAKE

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri Kiongozi kwa kuwa shughuli zetu za leo tulizozipanga zimekwisha naomba uliahirishe Baraza lako tukufu hadi kesho siku ya Alhamis tarehe 22-10-2009 saa 3:00 asubuhi. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kabla sijaahirisha kikao hiki naomba niwakumbushe tu kwamba kipindi cha maswali tumemaliza na tulikubaliana kwamba mara baada ya kipindi cha maswali basi ile semina ya Wizara ya Afya kuhusu madawa ya kulevya na Benki ya Damu itakuwepo ndani ya ukumbi huu. Tunategemea tuanze saa 4:30 ili kuwaruhusu watendaji wetu waje waweke utaratibu ndio tuanze semina hiyo. Nawaomba sana basi tusitawanyike tukafika mbali ili saa 4:30 iwe tumerudi ndani ya ukumbi huu kuendelea na

semina hiyo. Pia wakati huo huo kama Mhe. Waziri wa Afya na watendaji wake hawajafika basi apate kuwasiliana nao ili waje wajipange kwa ajili ya kuanza semina hiyo.
Baada ya hayo sasa naahirisha kikao hiki hadi kesho tarehe 22-10-2009 saa 3:00 asubuhi.

(Saa 4:09 asubuhi Baraza liliahirishwa hadi tarehe 22-10-2009 saa 3:00 asubuhi)